



Tarehe: 23/09/2020

YAH: TANGAZO LA ZABUNI (LINARUDIWA)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anawatangazia wafanyabiashara na wazabuni (watu binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu, vilivyosajiliwa kisheria) kutuma maombi ya kuendesha biashara kwenye bustani za kupumzikia eneo la Tilla, Maduka Makubwa na eneo la viwanja vya Mashujaa Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Hivyo wenyewe nia na uwezo wa kufanya kazi hiyo wajitokeze kutuma maombi kwa Zabuni zifuatazo:-

Nambari ya Zabuni	Eneo la Zabuni	Ada ya Zabuni
LGA/085/2019/2020/NC/12 LOT 1	<ul style="list-style-type: none"> Kusimamia michezo ya Watoto, kuendesha biashara ya kuuza vinywaji baridi, chakula na biashara ya kukodisha eneo kwa shughuli za sherehe na hafla mbalimbali eneo la Tilla Kata ya Rahaleo Manispaa ya Mtwara Mikindani. 	Shilingi elfu ishirini tu (20,000/=)
LGA/085/2019/2020/NC/12 LOT 2	<ul style="list-style-type: none"> Kuendesha biashara ya kuuza vinywaji baridi, chakula na biashara ya kukodisha eneo kwa shughuli za sherehe na hafla mbalimbali eneo la Maduka Makubwa Kata ya Shangani Manispaa ya Mtwara Mikindani. 	Shilingi elfu ishirini tu (20,000/=)
LGA/085/2019/2020/NC/12 LOT 3	A. Kuendesha bwawa la kuogelea(swimming pool)	Shilingi elfu ishirini tu (20,000/=)
LGA/085/2019/2020/NC/12 LOT 4	B. Biashara ya kuuza vinywaji vya aina zote kwenye bar, pub na cafe ya vinywaji baridi.	Shilingi elfu ishirini tu (20,000/=)
LGA/085/2019/2020/NC/12 LOT 5	C. Biashara ya kuuza chakula (mgahawa na mama lishe) Shughuli zote tajwa hapo juu zitaendeshwa katika eneo la viwanja vya Mashujaa.	Shilingi elfu ishirini tu (20,000/=)

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

Maombi ya Zabuni yazingatie Masharti yafuatayo:-

1. Nyaraka ya zabuni inapatikana baada ya kulipa ada ya zabuni ambayo haitarejeshwa na nakala ya stakabadhi iambatanishwe kwenye maombi.
2. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani ya mwombaji, aidha ataje mahali anapopatikana na namba zake za simu.
3. Mwombaji aoneshe mchanganuo wa maoteo ya mapato anayotarajia kukusanya, na kiasi atakacholipia Manispaa kwa Kila mwezi kwa biashara atakayoifanya.
4. Mwombaji atatakiwa kuambatanisha kivuli cha leseni ya biashara iliyo hai kama anayo, kivuli cha usajili wa Kampuni na nguvu ya kisheria (Power of Attorney), usajili wa VAT/TIN, na "Company profile" ya kampuni husika.

ZINGATIO: nguvu ya kisheria (Power of Attorney) ni kwa Kampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vilivyosajiliwa kisheria.

5. Mwombaji atalipa tozo itakayokubalika na atafanya usafi eneo lake la biashara kwa kuzingatia taratibu za Maafisa Afya wa Manispaa.
6. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.
7. Kabrasha la Zabuni linapatikana katika ofisi ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.
8. Maombi yafungwe kwenye bahasha ya khaki (A4) yenge lakiri – Zabuni iandikwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa,
S.L.P 92,
MTWARA-MIKINDANI.

9. Maombi ya zabuni yawasilishwe katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni Kitengo cha Manunuzi Makao Makuu ya Manispaa.

Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 06/10/2020 saa 5:00 asubuhi na ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni na wawakilishi watakaoamua kuhudhuria ufunguzi huo wanakaribishwa.


COL. Emmanuel Mwaigobeko
MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA - MIKINDANI

MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA - MIKINDANI
S. L. P 92
MTWARA